



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI
JESHI LA POLISI TANZANIA**



Simu No: 0739 034 304
Email: rpc.rufiji@tpf.go.tz

Ofisi ya:-
Mkoa wa Kipolisi Rufiji
Kamanda wa Polisi
S. L. P. 14
IKWIRIRI - RUFJI
13/03/2023

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Ndugu Wanahabari.

Mnamo tarehe 12/03/2023 majira saa 19:00hrs huko katika Kijiji cha Bweni na Kijiji cha Kanga, kata ya Kanga tarafa ya Kaskazini, Wilaya ya Mafia na Mkoa wa Kipolisi Rufiji, watu saba toka kutoka kaya nne tofauti walibainika kufa baada ya kula nyama ya samaki aina ya kasa anayesadikiwa kuwa na sumu.

Majina ya waliofariki katika tukio hilo ni kama wafuatao:- **1.** Abdalla s/o Hatibu Nyikombo, 4yrs, Mshirazi na mkazi wa Bweni **2.** Makame s/o Hatibu Nyikombo, 9yrs, Mwanafunzi S.t.d II S/Msingi Bweni **3.** Mohamedi s/o Juma Makame, miezi 7, Mshirazi na mkazi wa Bweni **4.** Ally s/o Selemani, miezi 8, mndengereko na mkazi wa Kanga **5.** Salima d/o Omary Mjohi, 28yrs, Mshirazi, Mkulima na mkazi wa Bweni **6.** Minza d/o Juma Hatibu, miezi 10, Mndengereko na mkazi wa Bweni na **7.** Ramadhani s/o Karimu, miezi 8 Mndengereko na mkazi wa Bweni, aidha marehemu hao walifariki majira tofauti tofauti katika tarehe tajwa hapo juu.

Miili ya marehemu imefanyiwa uchunguzi wa Kitabibu katika hospitali ya Wilaya Mafia na kukabidhiwa kwa ndugu kwa ajili ya taratibu za mazishi. Chanzo cha tukio hilo bado kinaendelea kuchunguzwa. Watuhumiwa watatu wanashikiliwa na Jeshi la Polisi Wilaya Mafia kwa mahojiano zaidi, katika hatua hiyo watuhumiwa hao wamelazwa katika hospitali ya Wilaya ya Mafia baada ya kuzidiwa wakiwa chini ya uangalizi wa Jeshi la Polisi, kwani nao walikula nyama ya samaki huyo.

Wito: Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi Rufiji anatoa wito kwa wavuvi Wilaya ya Mafia kuacha tabia ya kuvua samaki aina ya kasa ambao ni nyara za Serikali, bali wafuate taratibu na sheria za uvuvi wa samaki hawa, Jeshi la Polisi litaendelea kuchukua hatua kali kwa wavuvi wasiofuata taratibu na sheria za nchi.

IMETOLEWA NA:-

CANUTE S. MSACKY - ACP

Kaimu Kamanda wa Polisi

Mkoa wa Kipolisi Rufiji.